

**MKATABA WA KUKODISHA ENEO**

**KATI YA**

**SERIKALI YA KIJJI CHA NYANG'OMBE**

(Mpangishaji)

**NA**

**YAYO MINING COMPANY LIMITED**

(Mpangaji)

MKATABA HUU WA KUKODISHA ENEO umefanyika tarehe **10 JULAI, 2024**

KATI YA

**SERIKALI YA KIJJI CHA NYANG'OMBE** Anwani: S.L.P 113, MKOA: SHINYANGA, WILAYA: NYANG'OMBE, MTA: ISONDA, Tanzania (ambapo itajulikana kama "Mpangishaji", ambapo neno hilo litamaanisha pia mrithi wa umiliki kutoka kwa Mpangishaji, mrithi wake wa kisheria, na waliokubaliwa kupewa) kwa upande mmoja;

**NA**

**YAYO MINING COMPANY LIMITED** ya Dar es Salaam, Tanzania (ambapo itajulikana kama "Mpangaji", neno hili likiwahusisha warithi na wawakilishi wa mpangaji inapohitajika) kwa upande wa pili; pande zote zitatajwa kwa pamoja kama "Pande."

A. Kutokana na kuwa Mpangishaji ndiye mmiliki halali wa eneo lililopo katika **MKOA: SHINYANGA, WILAYA: NYANG'OMBE, MTA: ISONDA**, na kwa kuwa Mpangishaji ana nia na yuko tayari kukodisha sehemu hiyo kwa mujibu wa masharti na vigezo vilivyoainishwa hapa chini.

SASA HIVYO, Hati hii inashuhudia yafuatayo:

**INAKUBALIWA KWA PAMOJA KAMA IFUATAVYO:**

1. Mpangishaji atafanya yafuatayo:

a) Mkataba huu wa kukodisha utakuwa kwa kipindi cha miaka mitano (5), kuanzia tarehe **10 JULAI, 2024**, kama ilivyoainishwa kwenye Mkataba wa Kukodisha kati ya **SERIKALI YA KIJJI CHA NYANG'OMBE** na **YAYO MINING COMPANY LIMITED**, ambao utapitiwa kila baada ya miaka mitano.

b) Kodi ya eneo hili ni **shilingi milioni mia tatu (300,000,000)** tu, inayolipwa mapema kwa kipindi cha miezi ishirini na nne kuanzia tarehe **10 JULAI, 2024**.

2. Mpangishaji anakubali kwamba mpangaji atatumia eneo lililokodishwa bila kuingiliwa na Mpangishaji, wanafamilia wake, au wafanyakazi wake kwa kipindi cha miaka mitano mingine.
3. Ikifika mwisho wa kipindi cha miaka mitano ya awali, Mpangaji atafanya majadiliano mapya au mapitio ya masharti yanayofaa kwa upya wa mkataba kwa kipindi cha miaka mitano zaidi.
4. Eneo hilo litatumika kwa mradi wa usindikaji madini.
5. Pande zinazohusika zimesaini Mkataba huu wa Kukodisha katika tarehe na mwaka ulioainishwa hapa chini.
6. Mkataba huu wa KUKODISHA utatawaliwa na kufasiriwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania zinazohusiana na mahusiano ya mpangaji na mpangishaji kama zitakavyokuwa kwa wakati huo.
7. **Mpangishaji na Mpangaji wamekubaliana**  
Mwisho wa kipindi cha miaka mitano (5) ya kukodisha, Mpangaji atahitajika kununua mali iliyokodishwa kutoka kwa Mpangishaji. Pande zote mbili zinakubaliana kwamba bei ya ununuzi itakubaliwa kwa pamoja wakati wa ununuzi, kulingana na thamani ya soko itakayokadiriwa na wakadiraji huru. Iwapo Mpangaji hatakuwa na nia ya kununua mali hiyo, Mpangishaji atakuwa na haki ya kukodisha mali hiyo kwa mpangaji mwingine au kuiza kwa mnunuzi mwingine.

**KWA USHAHIDI HUU**, pande zote zinazohusika zimesaini Hati hii siku na mwaka ulioainishwa hapa chini:

IMESAINIWA NA KUWASILISHWA  
**SERIKALI YA KIJJI CHA NYANG'OMBE**

MWENYEKITI  
SERIKALI YA KIJJI NYANG'OMBE  
S.L.P. 113 SHINYAIGA

.....  
.....

**(Mpangishaji)**

Tarehe 10 JULAI, 2024

IMESAINIWA NA KUWASILISHWA  
**YAYO MINING COMPANY LIMITED**

.....  
.....

**(Mpangaji)**

Tarehe 10 JULAI, 2024

